



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA



Barua zote ziadikwe kwa:  
Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya  
Simu nambari: +255 (026)- 2702585/2702828  
Nukushi, +255(026)-2701776/2700580/270175

S.L.P. 108,  
IRINGA.  
TANZANIA

Barua pe ded@iringadc.go.tz

Tovuti: www.iringadc.go.tz

**TANGAZO**

**02.01.2025**

**FURSA ZA UWEKEZAJI KWA MFUMO WA UBIA (PPP)**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Iringa inawatangazia na kuwalishwa Wananchi Watanzania na wasio Watanzania, Taasisi, Mashirika, Kampuni, Wafanyabiashara na wadau wa maendeleo mbalimbali kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ina maeneo mbalimbali yanayohitaji uwekezaji wa aina mbalimbali kwa utaratibu wa ubia.
2. Mpango huu wa uwekezaji unajia na kutekelezwa kwa kuzingatia sera ya Ubia baina ya Sekta Umma na Sekta Binafsi (PPP), Sheria ya PPP ya mwaka 2010 Sura ya 103 na kanuni za mwaka 2020 pamoja na marekebisho yake. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa iko tayari kupokea aina nyingine yoyote ya mawazo ya uwekezaji ambao utakuwa tofauti na mpango huu wa ubia (PPP) kwa manufaa ya pande zote mbili katika uwekezaji tarajiwa.

**3. Maeneo hayo yanayotangazwa ni yafuatayo;**

S/N.	Eneo/Mahali	Ukubwa	Pendekezo la Biashara/aina ya uwekezaji
1.	Mboliboli/Mbugani	11,579 Acres	Eneo hili linafaa kwa; <ul style="list-style-type: none"> <li>- Kilimo cha <b>Miwa</b> na Mpunga</li> <li>- Ujenzi wa Kiwanda kikubwa cha <b>Sukari</b></li> <li>- Ujenzi wa Kiwanda kikubwa cha Mpunga</li> </ul>
2.	Mlenge/Magombwe	10,809 Acres	Eneo hili linafaa kwa; <ul style="list-style-type: none"> <li>- Kilimo cha <b>Miwa</b> na Mpunga</li> <li>- Ujenzi wa Kiwanda kikubwa cha <b>Sukari</b></li> <li>- Ujenzi wa Kiwanda kikubwa cha Mbunda</li> </ul>

3. Mseke/Ugwachanya 72 Acres -Eneo hili linafaa kwa ajili ya Ujenzi wa Viwanda Vikubwa na vya kati (Industrial Park/Zone)
4. Kising'a/ Igingilanyi 28 Acres Eneo hili lipo jirani na uwanja wa Ndege wa Iringa ( Nduri Airport) pembezoni mwa barabara kuu ya Iringa Dodoma, linafaa na kupendekezwa kwa ajili ya;
- Kituo kikubwa cha Mafuta na Mgahawa wa barabarani
  - Kumbi za kisasa (convention centre and multipurpose Conference Halls)
  - Sehemu ya Mapumziko na burudani (Recreational and Entertainment Centre)
  - Nyumba za Kupangisha/Apartments/ Hotels
5. Tungamalenga/  
Ruaha NPark 50 Acres Eneo hili lipo pembezoni mwa pori tengefu la MBOMIPA na Mbuga ya Wanyama ya Ruaha, linafaa na kupendekezwa kwa;
- Ujenzi wa Hotel za kisasa za kitalii
6. Makorongoni/  
Iringa Manispaa 6500 sqm Eneo hili linafaa kwa;
- Ujenzi wa Apartments na nyumba za kupangisha
  - Sehemu za Mapumziko na Burudani(Recreational and Entertainment)
  - Migahawa mikubwa ya kisasa
  - Malls and Departmental Stores
  - Governmental and Private Organizations Offices
7. Nduli 28 Acres Eneo hili lipo pembezoni mwa uwanja wa nudge wa Nduli, linafaa kwa;
- Ujenzi wa Hotel za kisasa za kitalii
  - Ujenzi wa Apartments na nyumba za kupangisha
  - Sehemu za Mapumziko na Burudani(Recreational and Entertainment)

- Migahawa mikubwa ya kisasa
- Kumbi za kisasa (convention centre and multipurpose Conference Halls)

8. Mawindi/ Nyang'oro 2000 Acres Eneo hili lipo pemezoni mwa Milima ya Nyang'oro na linafaa kwa;

- Ujenzi wa Kiwanda cha Saruji na malighafi zake
- Ujenzi wa Kiwanda cha Chokaa

4. Maeneo yote haya yapo katika ukanda na na hali ya kufikika na yenye miundombinu inayoshabihana na shughuli tarajiwa kama barabara, maji na umeme. Kwa maeneo yaliyopo ndani ya Manisapaa ya Iringa yapo karibu na maeneo ya yanayooa huduma za msingi kama Hospitali, Stendi za Mabasi, Masoko na Taasisi za Kifedha sambamba na huduma zingine za kijamii na Serikali.

5. Masuala mengine ya kuzingatia:

- Utaratibu huu wa Ubia (PPP) ni mawazo ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Mbia au ye yeyote mwenye nia anaweza kuona na kuwasilisha wazo lake tofauti na aina hii ya uwekezaji kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya na hivyo kutoa nafasi ya kujadiliana zaidi kwa manufaa ya pande zote shirika.
- Mradi utazingatia thamani ya fedha ikilinganishwa na utekelezaji wa Mradi kwa ununuzi wa kawaida unaotumia bajeti ya serikali (Kanuni ppp)
- Kwa yeyote mwenye nia na uhitaji wa kuwekeza kwa utaratibu huu au utaratibu mwengine wowote basi awasilishe Barua ya kusudio/nia (Expression of Interest) sambamba na wazo la Mradi (Concept note).
- Kwa mawasiliano zaidi, fika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Iringa iliyopo Njia Panda ya Mgama, kijiji cha Ihemi au tumia anuani ifuatayo;

**Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya ya Iringa  
S. L. P 108,  
Ihemi, IRINGA.**

OR ded@iringadc.go.tz/uwekezaji@iringadc.go.tz

*ROBERT M. MASUNYA*  
*MKURUGENZI MTENDAJI*  
*IRINGA HALMASHAURI YA WILAYA*  
*IBINGA*